# Mutazamo kuhusu mahitaji na mapendekezo ya jamii

## Watu wanahitaji njia bora za kuripoti vitendo na unyanyasaji wa kingono katika huduma za kibinadamu mashariki ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kupata habari kuhusu njia hizo mu luga zenye wanaelewa

Ripoti ya utafiti

Januari 2022

CLEAR Global

Translators without Borders

# Yanayo patikana ndani

**Habari kwa kifupi: kile unacho hitaji kabisa kujua. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3**

**Tulitaka kujifunza kutoka kwa wahanga wa unyanyasaji na watu ndani ya jamii kuhusu namna yabo ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 5**

**Matokeo muhimu: Njia za kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono haziendani kabisa na mahitaji ya mawasiliano ya wahanga, wasiwasi wa kukosa usalama na kutegemea kuishi kwa kufanya ngono . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6**

**Shukrani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 24**

**Vyanzo vilivyo tumiwa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 25**

**Kiambatisho 1: Vifupisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 27**

**Kiambatisho 2: Ukusanyaji wa habari katika utafiti. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 27**

## Oroza ya picha

Picha ya 1: Siyo kila wakati matokeo ya ripoti inaambatana na matarajio ya wahanga wa zuluma na unyanyasaji wa kingono mu jimbo ya Kivu ya Kaskazini. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 9

Picha ya 2: Karte iliyo tayarishwa na TWB kuhusu luga zinazo tumikishwa kwenye njia za simu jimboni Kivu ya Kaskazini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .13

Picha ya 3 : Luga kuu inayo zungumuzwa na wauzuriaji katika utafiti ndani ya jamii . . . . . . . . . .14

Picha ya 4: Luga zingine zinazo zungumuzwa na wauzuriaji katika utafiti ndani ya jamii . . . . . . . .14

Picha ya 5: Markasi za kubandikwa zinatowa maelezo kuhusu namba za simu zilizo wekwa na mashirika ya kibinadamu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .16

Picha ya 6: Watu ndani ya jamii hawakuelewa picha inayo onesha zuluma na unyanyasaji wa kingono . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .17

Picha ya 7: Picha kama hizi zinaweza kuongeza hali ya kujisikia kuzarauliwa kwa wanamuke ambao wanafanya ngono juu wapate gisi ya kuishi. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .18

Picha ya 8: Picha zinaonesha zuluma na unyanyasaji wa kingono kama tendo ya bila makubaliano zilieleweka muzuri. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .18

Picha ya 9: Kartasi ya kubandikwa inajulisha jamii juu ya haki yake ya kupata misaada ya kibinadamu bila kuzulumiwa na kunyanyaswa kingono, lakini haitowi maelezo kuhusu fasi ya kuripotia zuluma na unyanyasaji wa kingono . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .19

Picha ya 10: Mara mingi namna wahanga wana ripoti ni tofauti sana na namna yenye wanatarajia. .21

Picha ya 11: Gisi mfano muzuri inavyo onekana kwa muhanga (mfano ya utafiti) . . . . . . . . . . . 22

Picha ya 12: Washiriki katika utafiti ndani ya kila eneo kwenye utafiti ulifanyika . . . . . . . . . . . . 29

## Habari kwa kifupi: kile unacho hitaji kabisa kujua

Huu utafiti inachunguza ni kwa kiwango gani njia ya kuripoti na kutowa huduma kuhusiana na zuluma na unyanyasaji wa kingono (SEAH) mashariki mwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (RDC) haziambatani na mahitaji ya jamii na ya wahanga wa unyanyasaji. Inachunguza pia luga, mipangilio na njia za mawasiliano zinazo tolewa katika mifumo ya sasa na kuzilinganisha na mahitaji ya jamii. Watafsiri wasiyo na Mipaka/CLEAR Global walifanya huu utafiti pamoja pia na msaada kipesa ya Shirika la Afya Duniani.

Katika eneo ndogo (Petit-Nord) ya jimbo ya Kivu ya Kaskazini, wanamuke, wanaume na wafanyakazi wa mashirika ya kutowa misaada wana tambua vizuwizi mingi kwa kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono. Hivi vizuwizi vinahusiana na vikwazo vya kiuchumi; mawasiliano mubaya; namna ya kulenga wahanga, ukosefu wa ubora na usalama wa njia za kuripoti; na hatari ya kibinafsi:

1. **Mwanamuke kutojitegemea kipesa ni sababu kubwa ya hatari ya zuluma na unyanyasaji wa kingono.** Wanamuke wengi wanaingia katika mahusiano na watumishi wa mashirika ya kibinadamu kwa sababu hawajitegemeyi kipesa. Mara mingi wanapata faida ya pesa kwenye mahusiano kama hiyo, kwa hivyo siyo vyepesi kuripoti hiyo mahusiano kama zuluma na unyanyasaji wa kingono kwenye shirika ya kutowa misaada. Mara mingi habari inayo lenga kuzuwia zuluma na unyanyasaji wa kingono haizingatii iyi jambo na haitowi maelezo kuhusu faida za kuripoti. Wanamuke wanao fanya ngono juu ya kuishi waliomba msaada wa kipesa kama ipasavyo.

2. **Watu ndani ya jamii wanasema inaweza kuwa vigumu kuripoti muzuri zuluma na unyanyasaji wa kingono na kwa usalama.** Kuna wanamuke wenye hawana simu za mukononi; watu wanaripoti kwamba mara mingi wakipiga ku namba za simu hazijibiliwi; na wanamuke wanaripoti kwamba sanduku za maoni zinapatikana hazarani kwenye fasi ya watu wengi . Obuvu wa chombo cha sheria kwa kuweza kufatilia muzuri mashtaka kutokana na unyanyasaji wa kingono ina sababisha pia watu kutokuamini njia ao mfumo wa kutowa huduma. Na hiyo inapelekea wahanga kujikuta kwenye hatari wakati wa kuripoti unyanyasaji, ikiwa ni pamoja na kulipishwa kisasi. Usalama wa njia zinazo patikana za kutowa huduma zinapashwa kuchunguzwa na kuboreshwa na watu ndani ya jamii.

3. **Habari zinazo patikana zaidi kuhusiana na njia za kuaminika za kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono zinahitajika.** Siyo kila wakati watu wanajua gisi ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono kwa sababu habari kuhusu namna ya kuripoti haieleweki muzuri. Picha kwenye markasi ya kubandikwa zinatafsiriwa mubaya na habari mingi zinatolewa kwa Kifaransa, luga yenye watu wengi mu jimbo ya Kivu ya Kaskazini hawaelewi. Mara mingi vifaa vya kutowa habari havijibii maulizo ya msingi ya watu kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono na havina ushauri inayo faa kuhusu musaada yenye inapatikana.

4. **Juhudi za kutowa habari kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono zinahitaji kulenga vikundi vingine vyenye kuwa katika hatari – ikiwa ni pamoja na wanaume na vijana – pamoja na wanamuke wazee.** Kutozingatia hivi vikundi inaweza kusababisha watu kutojuwa wapi kwa kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono wakati inatokea. Wanahitaji njia za kuripoti na kampeni za uhimizaji zenye zina ambatana na mahitaji yao ya mawasiliano na hatari ya kujisikia kuzarauliwa.

## Mapendekezo

Kwa hiyo, tunapendekeza kwamba mashirika za kutowa misaada zishirikiane na wanamuke na wanaume kwa kuweza kufanya njia ya kuripoti kuwa salama na rahisi zaidi kutumia. Mashirika zinaweza kukamata hatua zifwatazo juu ya kuambatanisha namna yao ya kutumika na mahitaji ya jamii kuhusu kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono:

1. **ReKuchunguza mara ya pili na kuboresha njia zenye ziko za kuripoti.** Kushirikiana na jamii ili kuchunguza mara ya pili matumizi na usalama wa njia zenye ziko za kuripoti. Kufukuza na kuripoti watowa huduma na viongozi wanao fanya unyanyasaji. Kuboresha matumizi ya masanduku ya maoni kwa ajili ya kuripoti kwa siri kwa kukagua mara kwa mara na kujibia malalamiko ao mapendekezo. Kuhusu namba za simu, kuhakikisha kwamba simu zinajibiliwa na kwamba huduma zinapatikana katika luga za nyumbani zinazo faa. Kama watu hawawezi kutumia njia za kuripoti zenye zinapatakinana, washirikiane nao juu ya kupata njia zingine zinazo faa.

2. **Kuweka na kusaidia njia salama za kuripoti zenye zinawezesha wahanga kuripoti uso kwa uso ao kwa msaada wa mtu wanaye amini.** Kutoa mafunzo na msaada wa kipesa wa kuendelea kwa mipango ya wanamuke na jamii ili kuunga mukono wahanga kama sehemu ya njia salama za kuripoti na njia za kufuatilia kesi. Kwa muda mrefu, mashirika ya kutowa misaada zinapashwa kusaidia kuimarisha mfumo wa sheria wa Kongo ili kuhakikisha wahanga wa zuluma na unyanyasaji wa kingono waweze kuripoti kwa usalama na wanyanyasaji wafatiliwe na kuazibiwa.

3. **Kuboresha utowaji wa habari kuhusu namna ya kuripoti muzuri zuluma na unyanyasaji wa kingono kwa usikilivu bora.** Kuonesha jamii njia tofauti za kuripoti zenye inaweza kutumikisha. Kutowa habari muhimu kuhusu utaratibu wa kuripoti na msaada yenye wanaume, wanamuke na watoto wanaweza kupokea. Kutosha matangazo (affiches) zenye zinapana namba za simu zenye hazitumiki ndani ya jamii. Kuhakikisha habari inapatikana katika luga za nyumbani na kujaribu kwanza kutumia maandiko na picha ndani ya jamii kwa usikilivu na kukubalika.

4. **Kuendeleza mbinu zinazo lenga wanaume, vijana na vikundi vingine vyenye kuwa katika hatari. Kutafuta vikundi vyenye kuwa katika hatari ambavyo haviyapata habari za sasa na kuhusu njia za kuripoti. Kutengeneza mbinu za kipekee juu ya kufikia hizi jamii ambazo zinazingatia shida zote zenye watu ndani ya hizi jamii wanapata (ikiwemo kujisikia kuzarauliwa) na njia za mawasiliano zenye wanapendelea. Mbinu zinapashwa pia kuzingatia kuhimiza tabia ya wanaume ya kusaidia wanamuke kuripoti mahusiano ya unyanyasaji na mahusiano ya mukazo**.

5. **Kusaidia kuzuwia zuluma na unyanyasaji wa kingono kwa kutowa msaada wa kimaisha na wa kujitegemea kiuchumi.** Hii inaweza kuambatanisha shuruli kuhusu mawasiliano inayo husiana na kukingwa na zuluma na unyanyasaji wa kingono na utumaji wa pesa. Mashirika za vijijini ya akiba na mkopo (AVEC) zinavuma siku hizi na zinaweza kuwa njia bora ya kusaidia wanamuke kipesa.

## Tulitaka kujifunza kutoka kwa wahanga wa unyanyasaji na watu ndani ya jamii kuhusu namna yabo ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono

Unyanyasaji wa kingono mashariki ya Kongo inaendelea kuongezeka na mara mingi unaripotiwa kufanywa na vikundi vyenye silaha na vikosi vya jeshi vinavyo patikana katika eneo fulani. zuluma na unyanyasaji wa kingono inafanywa pia wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu. Siku zilizo pita kuliripotiwa zuluma na unyanyasaji wa kingono ikiwemo unyanyasaji wakati wa muripuko wa 10 wa ugonjwa wa Ebola inchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika jimbo ya Ituri na Kivu ya Kaskazini[1]. Mashirika ya kibinadamu zina towa huduma kwa wahanga wa zuluma na unyanyasaji wa kingono katika hizi maeneo. Hata hivyo, mafasiriyo yao ya unyanyasaji wa kingono inaonekana kushawishiwa na mitazamo ya inchi za bulaya na inatowa maelezo kidogo kuhusu wanyanyasaji, wahanga na suluhisho zilizo chukuliwa kwenye ngazi ya kimataifa.[2]

### Tulikusanya maoni ya watu 124 mu jimbo ya Kivu ya Kaskazani

Tuliuliza wanamuke na wanaume, ikiwemo wahanga wa unyanyasaji wa kike na wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu, kuhusu mambo waliyo pitia kuhusiana na njia za kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono zilizo wekwa na mashirika ya kibinadamu, na maoni yao kuhusu umuhimu wa hizi njia.

Timu iliyo fanya utafiti ilitumia vifaa mbalimbali kama sehemu ya mbinu ya kupata maoni yenye ubora. Hivi vifaa ni pamoja na uchambuzi wa maandiko wa haraka; karte yenye liste ya ma luga, mipangilio na njia za kuripoti na kutowa huduma kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono; na ukusanyaji wa habari ya msingi kwa kushirikiana na watu katika jamii, wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada na wahanga wa zuluma na unyanyasaji wa kingono, kupitia mazungumuzo ya vikundi na mahojiano fupi iliyo pangwa.

Ukusanyaji wa habari za msingi ulifanyika zaidi ya juma tatu mashariki ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Katika yote, timu ya watafiti ilizungumuza na washiriki 106 katika jamii zenye zinapokea msaada katika maeneo mbili zilizo guswa na muripuko wa volkano ya Nyiragongo mwezi ya tano 2021, ikiwemo wahanga wa zuluma na unyanyasaji wa kingono uliyo fanyiwa na wafanyakazi wa kibinadamu. Pia walizungumuza na wafanyakazi 18 wa mashirika za kutowa misaada katika miji ya Goma na Beni.

Mapungufu kubwa ilitokea wakati ya kuendesha utafiti ni kwamba mashirika zilizo saidia kuwapata wahanga wa zuluma na unyanyasaji wa kingono zilipata wahanga wachache ndani na karibu ya Goma waliyo itika kushiriki. Wahanga wengi walikatala kushiriki kwa sababu ya kuogopa kujisikia kuzarauliwa ao juu ripoti waliyo fanya ya zamani haikutuma wanapata haki ao msaada kutoka kwa mashirika ya kutowa misaada. Mapungufu ingine ilikuwa kwamba katika muda mfupi wa utafiti, timu ya watafiti haikuweza kuzungumuza na wahanga wa kiume, vijana na watoto waliyo fanyiwa zuluma na unyanyasaji wa kingono na watumishi wa mashirika ya kibinadamu.

---

[1] Tembelea: https://www.thelancet.com/journals/lancet/article/PIIS0140-6736(21)02214-5/fulltext.
[2] Tembelea: https://www.jstor.org/stable/41494485

## Matokeo muhimu: Njia za kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono haziendani kabisa na mahitaji ya mawasiliano ya wahanga, wasiwasi wa kukosa usalama na kutegemea kuishi kwa kufanya ngono

### Wahanga wanaweka siri kuhusu mahusiano yao na wafanyikazi wa mashirika za kutowa misaada kwa sababu hawaioni kama zuluma na unyanyasaji wa kingono ao kwa sababu wanaogopa vinyume ya kuripoti

Wanamuke waliyo shirika katika huu utafiti hawakuona mahusiano ya kingono na watumishi wa mashirika ya kibinadamu kama unyanyasaji, kutendewa mubaya ao kusumbuliwa. Kwa kweli, mahusiano mingi na watumishi wa mashirika ya kibinadamu zilionekana kama zenye kufanyika kwa makubaliano, za muzuri na mara nyingi zenye kuwa na faida. Mama mumoja mukulima alirudia maoni ya wengi na kusema: *"Ukiingia katika mahusiano na mutumishi wa shirika ya kibinadamu uko na bahati, ni kama zawadi kutoka kwa Mungu."* Mahusiano na wafanyakazi wa mashirika ya kibinadamu walionekana kuwa muhimu kwa ajili ya maisha, wanamuke walieleza: *"Bila hiyo, watoto hawatapata kitu yoyote ya kukula."* Iyi matokeo ni kama matokeo ya utafiti ingine iliyo fanyika inchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.[3]

Kwa upande ingine, watumishi wa mashirika ya kibinadamu wanaona mahusiano kama hiyo kati ya watowa misaada na wanao pokea misaada kama tatizo na tendo ao jambo inayo katazwa. Hata kama mafasiriyo ya maneno muhimu inayo husiana na zuluma na unyanyasaji wa kingono zinatofautiana kati ya mashirika za kutowa misaada, zote zinaonesha zuluma na unyanyasaji wa kingono kama mahusiano isiyo kuwa na malamka ya sawasawa, mara mingi inahusisha nguvu, mukazo na ukosefu wa makubaliano.[4] Iyi tofauti ya mutazamo ni shida kubwa yenye inatuma watu hawaripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono. Wanamuke hawazoweyi kuripoti mahusiano ya unyanyasaji na watumishi wa mashirika ya kibinadamu kwa sababu hawaoni kama hizo mahusiano zina leta shida yoyote.[5]

### Wanamuke na mabinti wanaweza kusita kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono kwa sababu ya hatari mingi katika jamii zao

Wanamuke wengi wenye walihojiwa ndani na karibu ya Goma walisema kwamba hawawezi fichua mahusiano yao na mutumishi wa shirika ya kibinadamu kwa mtu yeyote. Hivyo njo gisi ilikuwa kwa wanamuke waliyo olewa na wenye hawayaolewa. Siyo tu kwamba hawakuripoti kwenye shirika ya kutowa misaada; wanamuke waliweka pia mahusiano kuwa siri mbele ya ba bwana yabo, familia na jamii yote. Kama gisi mwanamuke mumoja mkulima aliye olewa alisema: "Ningekuwa na mahusiano kama ile, ningeiweka mu roho yangu na singe ambia mtu yeyote." Sababu ni rahisi: wanamuke wanajikuta katika hatari kubwa kama wanaripoti.

---

[3] Utafiti uliyo fanyika siku kidogo zilizo pita na Cellule d 'Analyse Intégrée (CAI, iliyo julikana kama CASS), katika jimbo la Equateur, inchini Kongo, inaonesha pia kukubalika sana ndani ya jamii shuruli za ngono zinazo husisha wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada. https://www.unicef.org/drcongo/media/5901/file/COD-CASS-Equateur-PSEA-EN-correction.pdf

[4] Tazama kanuni sita za msingi kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono kutoka Kamati ya kudumu ya ushirikiano wa mashirika (Inter-agence) hapa: https://interagencystandingcommittee.org/system/files/iasc_six_core_principles_relating_to_sexual_exploitation_and_abuse_2002.pdf

[5] Mwaka 2015, vituo vya mawasiliano ndani ya jamii inchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo viliripoti pia kwamba *"jamii haikuona unyanyasaji wa kingono kuwa unyanyasaji "kwa kweli"*. Tembelea: https://interagencystandingcommittee.org/system/files/2021-03/Best%20Practice%20Guide%20Inter%20Agency%20Community%20Based%20Complaint%20Mechanisms.pdf

Kutaka kulinda siri inaeleweka: wanamuke walisema kwamba mahusiano kama hiyo na mutumishi wa shirika ya kibinadamu inajulikana, wanaweza kuzarauliwa, kupoteza mali na hata kufanyiwa unyanyasaji wa kimwili.

Viongozi wa jamii wa wanaume katika jamii moja walizibitisha kwamba wanamuke wanaweza kupigwa kama wanaripoti unyanyasaji kwa shirika ya kutowa misaada. Kiongozi mumoja mzee wa jamii alisema: "Tutamupiga kama anazungumuza hiyo jambo mbele ya shirika fulani." Wengine viongozi ine wa kiume wenye walikuwa pale walimupigia mikono wakati alifasiria juu ya nini: "Kama siyo hivyo, siye bote hatutapata misaada." Iyi inaweza kuwa maoni ya jamii fulani, ambapo tuliambiwa ukosefu wa usalama inapunguza kiwango ya kutowa misaada. Hata hivyo, hiyi inaonesha kiwango ya hatari ya kipekee ambayo wanamuke wanaweza kuwa amo kama wanaripoti unyanyasaji wa kingono.

Vinyume kwa wanamuke vinaweza kutokana pia na hali yao ya ndoa.

## Wanamuke wenye wanaolewa wanaweza kuzarauliwa na kupoteza mali na familia zao kama wanaripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono

Wanamuke wenye wanaolewa na kupatikana katika mahusiano na watumishi wa mashirika ya kibinadamu hawawezi kuripoti kila wakati mbele ya mashirika ya kutowa misaada kwa sababu wanaogopa kupewa talaka, kupoteza mali na kuzarauliwa kama familia ao jamii inagundua. Kuna watu ndani ya jamii wenye walituambia kama wanamuke wenye wanaolewa ambao wanashakiwa kuwa na mahusiano na shirika ya kibinadamu wanaweza kuletwa katika familia ya ba bwana yabo juu wazazi wa bibi na bwana waweze kuzungumuzia suluhisho ya kipesa. Wanamuke walisema kwamba mwa hiyo mikutano, mara mingi wanamemba wa familia wanaunga bwana mukono, hata kama mwanamuke anaeleza kuwa hiyo mahusiano ilikuwa tu namna yake moya ya *"kukulisha watoto." "Wanawalaumu wanamuke,"* mwanamuke mumoja alisema. Mwanamuke mwingine alikubali: *"Wanasema wanamuke hawapashwi kumutongoza mwanaume."*

Wanamuke wenye wanaolewa walishiriki katika huu utafiti walielezea namna gani sasa wanaweza kuwa na iyi mahusiano kwa siri. Wanamuke wanatumia neno kisakoshe kumaanisha mutumishi wa shirika ya kibinadamu katika mahusiano na mwanamuke mwenye anaolewa.[6] Iyi neno inatafsiriwa moja kwa moja kama "mufuko ya mkubwa" ao "mufuko ya pesa". Kulinda "mfuko wa pesa" kwa siri mu konte (compte) ya mwanamuke: *"Unaambia bwana yako unaenda tafuta mboga inje… kama uko na* kisakoshe*, wakati unarudia, unaenda mu nyumba ya jirani na unamuuliza kama anaweza kukupigia mboga juu uoneshe bwana yako kama ulienda kutafuta mboga, ijapokuwa kwa kweli ulikuwa naenda kumuona kisakoshe juu watoto wapate kitu ya kula."*

Wanamuke wanasema kwamba wakati ba bwana yabo banabaunga mkono zaidi, hawahitaji musaada sana kutoka kwa kisakoshe. Kama vile mwanamuke ndani ya kijiji kwenye utafiti ulifanyika alisema: *"Wanaume wanatumia pesa kuuza tu pombe, lakini minahitaji kukulisha batoto."* Wengine walitowa malalamiko ya kwamba wanaume wanacheza michezo ya bahati (pari) wakati wanamuke *"wanaenda ku shamba kulima juu ya batoto yabo."* Wanaume wenye walishiriki katika huu utafiti waliomba wanamuke kuwa waangalifu sana na kukubali hali yao ya kipesa. Bengi baliripoti shida ya kupata kipato, hasa wakati wa janga ya ugonjwa wa korona. Wanamuke na wanaume walitambua kwamba kama wanamuke wangekuwa najitegemea zaidi kipesa, hawawezi hitaji *kisakoshe* anaye tumika katika shirika ya kibinadamu.

---

[6] Iyi neno inatumikishwa pia kumaanisha watu wengine matajiri.

### Wanamuke wenye hawayaolewa wanaweza kupoteza elimu, nyumba yao na kulazimishwa kuolewa

Wanamuke wenye hawayaolewa walituambia kama wanapata shida mbalimbali wakati wa kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono. Wanamuke ndani ya vijiji kwenye utafiti ulifanyika walisema wanaweza kulazimishwa kuolewa na munyanyasaji wabo kisha familia kulipwa kwa njia ya mifugo. Wafanyakazi wa mashirika ya kutowa misaada walisema ya kwamba makubaliano yenye haiko rasmi kama hiyo zinaanza punguka katika jamaa zilizo elimika na maeneo ya miji katika Petit-Nord. Wanamuke vijana walituambia pia kwamba kama hiyo mahusiano inagunduliwa ao kama wanabeba mimba, wanaweza fukuzwa mu nyumba za wazazi yabo ao kuacha masomo.

## Wahanga wanaweza amua kutoripoti kwa sababu wanaamini kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono haitakuwa na matokeo muzuri na inaweza kuwa hatari

Wanamuke mingi walituambia hawaaminii kama kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono iko na matokeo muzuri kila wakati. Kwa ngambo moya iyi inatokana na hali yenye marafiki na familia walipitia, lakini hasa juu ya mifano ya wanamuke ndani ya jamii wenye walinyanyaswa na mwenye haiko mutumishi wa shirika ya kibinadamu. Muhanga mumoja wa zuluma na unyanyasaji wa kingono mara mingi alisema: “Nilibakwa, niliripoti, lakini sikupata suluhisho. Nilipoti juu ya nini?” Kama aina tofauti za unyanyasaji wa kingono ni kinyume ya sheria ya Kongo, ni mara kidogo sana wahanga wa unyanyasaji wa kingono mashariki mwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo wanapata haki.[7] [8] Wanamuke na watowa misaada ya kisheria waliyo shiriki katika huu utafiti wanasema ya kwamba taratibu za korti hazina uwazi na beyi za kufungula kesi ziko yulu sana.

Kutokana na iyi ukosefu kubwa wa haki, watu wanaona kuzungumuza juu ya zuluma na unyanyasaji wa kingono ni hatari, wanaogopa munyanyasaji asiweze kugeuka wa vurugu zaidi kama wanaripoti. Kama mufanya biashara mumoja, aliye olewa na watoto tatu, alieleza: *"Ndani ya siku tatu za munyanyasaji kwenda mu gereza atakuwa alisha achiliwa, na kisha unapashwa kuwa mwangalifu: anaweza tuma mtu akuye kukuuwa."* Kwa hiyo jamii na jamaa zinaweza kukatisha tamaa usiripoti.


Picha ya 1 inatumia mfano ya kesi yenye inaonesha matokeo ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono kama inavyo fikiriwa na watowa misaada, na byenye binazowea kutokea mara mingi. Vituo vya picha juu ya mfano ya kesi ya Carine. Carine siyo mtu wa kweli, lakini ni jina ya mtu iliyo tungwa. Kwa lengo ya iyi mfano, tunasema kwamba Carine anataka kuripoti unyanyasaji uliyo fanywa na mutumishi anaye towa huduma za kibinadamu katika jamii yake.

---

[7] Tembelea: https://www.fidh.org/IMG/pdf/rapport_rdc_.pdf
[8] https://www.jstor.org/stable/43904821 < ; https://ihl-databases.icrc.org/customary-ihl/eng/docs/v2_cou_cd_rule93

*Picha ya 1: Siyo kila wakati matokeo ya ripoti inaambatana na matarajio ya wahanga wa zuluma na unyanyasaji wa kingono mu jimbo ya Kivu ya Kaskazini*

## Njia rasmi iliyo wekwa na mashirika ya kutowa misaada:




*** Matokeo: utaratibu unasimama na hakuna haki kwa aliye fanyiwa unyanyasaji.**

## Wahanga wanataka kuripoti mahusiano ya unyanyasaji kwa siri kwa mtu mwenye wanaaminia, wa jinsia moja, lakini iyi haiwezekani kila wakati

Ijapokuwa hizi shida, wahanga wanaweza kuamua kuripoti kwa shirika ya kutowa misaada wakati wanaanza kuona kama hiyo mahusiano ni unyanyasaji. Hii inaweza kuwa wakati inakuwa ya kuleta usumbufu ao wakati ahadi kuhusu msaada wa kipesa inavunjika. Wahanga wanasema kwamba wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada na walinda amani wanawatelekeza pamoja na watoto wao wakati wanapata kazi mpya fasi ingine. Muhanga mumoja alizungumuza kuhusu uamuzi wake wa kuripoti: “Nilikuwa mufanya usafi kwake na tukaanza mahusiano. Alinilipia nyumba mwaka muzima lakini akaenda kwa gafla. Nilimwambia bosi yangu kuhusu hiyo.” Wahanga unyanyasaji wa kingono na ubakaji wanaripoti kwamba walijulisha wahudumu wa afya ili kupata msaada wa matunzo, hata kama waliogopa kuzarauliwa katika jamii yao. Muhanga mumoja alituambia: *“Aliniambia alikuwa na UKIMWI, ilibidi nipimwe.”*

Wahanga wa kike walisema kwamba wanapendelea kuripoti mahusiano unyanyasaji kwa wanamuke wenye wanaaminia, hasa mu luga yao. [9] Wahanga wote waliyo shiriki katika utafiti waliripoti kwanza shida zabo kwa rafiki wa kike ao ndugu wa jamaa *"mwenye minajua anaweza kulinda siri"* na kisha sasa kwa mutowa huduma wa kike wa kikongomani anaye aminika (mara mingi kulingana na jamii). Kati ya wahanga wenye tulizungumuza nabo, wengi walijulisha watowa huduma wanao zungumuza luga za nyumbani kwanza, na walipata matokeo muzuri zaidi kuliko wale wenye waliripoti kupitia sanduku za maoni na/ao namba za simu. [10]Wanamuke wenye waliripoti kwa watowa huduma wa kuaminika walidai kupata msaada na kueleweka.

## Siyo kila mara wahanga na watu ndani ya jamii zingine wanaaminia njia za simu na masanduku ya maoni kuwa bora na wakati ingine wanasita kuzitumia

Wahanga na watu ndani ya jamii zingine jimboni Kivu ya Kaskazini pia walieleza shida ya kutumia njia zenye ziko za kuripoti na walitowa maoni yao ya kuleta suluhisho.

### Wanamuke wanasema siyo salama kutumia masanduku ya maoni kwa kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono

Wanaume na wanamuke wanaeleza kwamba siyo salama kutumia masanduku zimoya zimoya za maoni kwa kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono. Muhanga alielezea gisi aliripoti kupitia sanduku ya maoni ya shirika ya kimataifa: *“Ali [munyanyasaji] fungua malalamiko yangu juu yake hapo hapo. Alijua kama ni miye. Ilikuwa ya kutisha sana.”* Alielezea boga yake ya kulipishwa kisasi na mutumishi wa shirika ya kutowa misaada, mwenye alimwambia alinde siri. Muhanga aliacha kazi yake na hajawahi tena kufanya kazi mu shirika (ONG) tangu hiyo siku. Wanaume na wanamuke wenye walishiriki katika huu utafiti mara mingi walitaja pia zingine shida kutokana na masanduku ya maoni. Hizi shida ni pamoja na kwamba masanduku ya maoni zina funguliwaka mara kidogo tu; kwamba ripoti hazijibiliwaki; na kwamba masanduku zina funguliwaka hazarani na "kamati inayo husika na malalamiko", na iyi ilileta shida sana ya kulinda siri wakati ya kuripoti.

[9] Hatukuzungumuza na wahanga wa kiume. Mashirika ya kutowa misaada zinazo tumika na wahanga wa unyanyasaji wa kingono wa kiume na wa vijana wanaume zinapashwa kuchunguza zaidi mahitaji ya wahanga wa kiume kuhusu namna ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono.
[10] Tafiti zaidi kuhusu gisi wahanga wanaripoti kupitia namba za simu, masanduku ya maoni na njia zingine zinazo tumiwa na mashirika ya kutowa misaada zinahitajika ili kuelewa muzuri iyi mambo.

Wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada pa Goma wana pendekeza kwamba masanduku ya maoni zenye ziliwekwa kwa makusudi mu fasi zenye wanamuke wana tembelea kama vile misarani (toillettes) za watu wote inaweza kuwa na matokeo muzuri. Wanaripoti pia kwamba katika maeneo zingine za Kivu ya Kaskazini mashirika zilipata suluhisho kwa hizi shida kwa kutumia masanduku ya maoni. Kwa mfano, katika maeneo ya Beni na Butembo iliyo kumbwa na ugonjwa wa Ebola mashirika ya kijamii ziko na kamati za wanamuke tu zinazo fungula masanduku mara kwa mara. Hawa wafanyakazi wanapendekeza kwamba mashirika zitafute mbinu zenye mafanyikio na kushirikisha wengine.

## Wanaume wanapenda kutumia njia za simu lakini wahanga wa kike wanapendelea kuripoti uso kwa uso

Wanamuke waliyo shiriki katika huu utafiti (pamoja na wahanga) hawakutaya namba za simu kama njia inayo pendelewa kwa kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono. Lakini, wanasema wangependa kuripoti kwa mwanamuke mwenye wanajua na kuamini (na siyo mutowa huduma asiye julikana ambaye hawajawahi kukutanana naye). Mutowa huduma mumoja kwenye njia ya simu alizibitisha kwamba mara mingi wahanga hawafichuwi kile kilicho watokea kwa njia ya simu. Alilazimika kukutana na wahanga uso kwa uso ili kufanya mazungumuzo ya maana, alisema: "Wanajisikia wasiwasi kumwambia mtu mwenye hawayawayi kukutanana naye." Mara mingi ana kutanana na wahanga kwa siri, kwa sababu wanaogopa kujisikia kuzarauliwa ndani ya jamii yao.

Wanaume wanasema wanapenda njia za simu kwa sababu wanazowea kupiga simu kwa mashirika ya kibinadamu kuripoti shida za wasiwasi bila kujulikana. Mashirika mingi inchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo zilianzisha vituo vya simu ambapo wateja kutoka mashirika za kutowa misaada wanaweza kuzungumuza na watowa huduma, ambao wana rikodi shida zao (kwa mfano, kuhusu musaada na mapokezi ya chakula). Wanaume wanasema wanazowea njia hizi na kwa sababu wanaweza kupiga simu (kwa bure) kuliko kutumia franga ya usafiri kwenda kwenye ofisi ya shirika. [11] Mutumishi mumoja anaye husika na unyanyasaji wa kingono pa Goma alizibitisha kwamba watu mingi wenye wanapiga simu kwenye ushirikiano wa mashirika unayo husikana zuluma na unyanyasaji wa kingono ni wanaume. Hata hivyo, wanaume waliyo shiriki katika utafiti hawakujua namba ya simu ya ushirikiano wa mashirika kwa ajili ya kuripoti vitendo na unyanyasaji wa kingono.

Wanamuke na wanaume waligundua pia shida ambazo zilisababisha matumizi ya njia za simu kwa kuripoti kutokuwa na mafanyikio sana. Wanamuke katika maeneo ya vijijini na kutoka jamaa maskini walisema hawana uwezo wa kutumia simu za mkononi. Wanaume walisema kwamba mara mingi njia za simu hazijibiliwi na kwamba watowa huduma wana ahidi kukuita na mara mingi hawaiti. Timu iliyo fanya utafiti iliweza kuzibitisha iyi jambo moja kwa moja. Tulipo wasiliana na njia za simu 11 ambazo zinatumiwa na mashirika zaidi ya 23 mashariki ya Kongo, mara mingi zinapokea simu mingi wakati wa kazi kabla ya simu kujibiwa. Mara mingi pia njia za simu hazitumiki inje ya saa za kazi za mashirika za kutowa misaada. Mara mingi wanamuke na wanaume wanapatikana ku mashamba zabo ao kufanya kazi ingine wakati wa masaa ya kazi kwenye ofisi na wanapendelea kuzungumuza na watowa huduma asubuyi, mangaribi ao mwisho ya juma.

---

[11] Njia zote za simu ambazo zinatumiwa na washirika wanao husika na kazi kuhusu unyanyasaji wa kingono Kivu ya Kaskazini zinatumika bila malipo. Tuliita vituo 44 vinavyo husika na unyanyasaji wa kingono mu jimbo ya Kivu ya Kaskazini kwa mashirika 23. Hizi mashirika zina tumia jumla ya njia 11 tofauti za simu juu ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono Kivu ya Kaskazini.

## Shida kwa wahanga wanao ripoti unyanyasaji ni kwamba mara mingi watowa huduma wa njia za simu mu inchi hawazungumuzi luga inayo faa katika eneo zinazo husika

Shida ingine ni kwamba mashirika zinazo towa huduma kwa njia ya simu mu inchi yote kutoka Kinshasa (ikiwemo namba ya simu ya kuripoti ako ya ushirikiano wa mashirika inayo husika na unyanyasaji wa kingono, 49 55 55) zinatowa habari mu luga rasmi ya inchi ao za kitaifa tu (tazama picha 2). Hizi njia za simu zinatumika mu Kifaransa, Lingala na Tshiluba (luga za kitaifa zenye watu mingi mashariki ya Kongo hawaelewi), na Kiswahili ya Kongo (ambayo watu mingi hawazungumuzi ao hawajisikia huru kuzungumuza). Washiriki mingi katika huu utafiti walisema wanapendelea kutowa na kupokea habari mu luga za nyumbani kama kikumu na kinande (tazama picha ya 3 na 4). Kuna wakati watowa huduma wanaweza pia jutowa habari mu luga zabo za nyumbani[12] lakini kwa kuwa vituo kama hivyo vinatumika kutoka muji mkuu (capitale) haiwezekani watowa huduma mingi kuzungumuza luga za nyumbani ao zile zenye zinazungumuzwa na watu wachache wa Kivu ya Kaskazini.

Mashirika mingi zinatowa huduma kuhusu unyanyasaji wa kingono katika Petit Nord, hasa mashirika zisizo za kiserkali za kitaifa, zinahimiza kutumia namba ya simu ya ushirikiano wa mashirika kutoka Kinshasa kwa kuripoti ya zuluma na unyanyasaji wa kingono (kwa kuita bila malipo namba 49 55 55). Mara mingi mashirika zisizo za kiserkali za kitaifa zina pendelea kuanzisha njia zao wenyewe za kupokea maoni ya jamii na kwa kutumia simu na kukabizi mutumishi ao watumishi kwenye timu zabo wenye wanazungumuza luga za nyumbani (mara mingi ofisa anaye husika na ufuatiliaji na uchunguzi ao ofisa wa ulinzi). Mashirika zingine zisizo za kiserikali zinatowa wito kwa vikundi vya mawasiliano vya kijamii na wafanyakazi jimboni Kivu ya Kaskazini juu ya kusaidia kutafsiri kwa kuandika ao kuongea, wamoya wanapewa mafunzo kuhusu unyanyasaji wa kingono na wengine hawapati. Hakuna shirika yoyote ile kati ya hizi ilikuwa natumia tafsiri wa kitaalamu kwa kuandika ao kuongea ao kupatia wafanyakazi jukumu ya kufanya hizi kazi kabla ya kupata mafunzo inayo faa.

Tuliambiwa kuhusu hali ambapo wanamuke hawakuweza kuripoti kwa usiri kwa njia za simu zinazo tumika kutoka Kinshasa ao kuelewa habari zenye zina tolewa kwa sababu luga yenye wanapendelea haitumikishwi. Mu hali kama hiyo watowa huduma kwenye njia za simu wanaomba mtu anaye piga simu atafute wa kumusaidia kutafsiri, ao wenyewe wanatafuta mwenzabo wa kazi mwenye anaweza kutafsiri. Iyi hali iliripotiwa na wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada jimboni Kivu ya Kaskazini na kuzibitishwa na habari kwenye karte katika huu utafiti. Siyo kila wakati njo wanatumia mtu wa kutafsiri katika hali kama hizi. Wafanyakazi wa mashirika ya kutowa misaada wanatambua kuwa wahanga wanaweza kujisikia kutoamini mtu wa kutafsiri mwenye hawajui ao mtu ndani ya jamii ingine kwa kutafsiri habari ya kisiri kama hiyo.

[12] Wakati wa kutayarisha karte ya luga, kwa mfano, tulizungumuza na muzungumuzaji wa kinande anaye ishi Kinshasa.


*Picha ya 2: Karte iliyo tayarishwa na TWB kuhusu luga zinazo tumikishwa kwenye njia za simu jimboni Kivu ya Kaskazini*

| # | Inatumika na | Luga zenye zinatumikishwa rasmi na njia ya simu |
|---|---|---|
| 1 | ONU | Kifaransa, Kiswahili, Tshiluba, Lingala |
| 2 | ONGI | Kifaransa, Kiswahili |
| 3 | ONGI | Kifaransa, Kiswahili, Tshiluba, Lingala |
| 4 | ONGI | Kifaransa, Kiswahili, Tshiluba, Lingala |
| 5 | ONU | Kifaransa, Kiswahili, Tshiluba, Lingala |
| 6 | ONU | Kifaransa |
| 7 | ONG | Kifaransa, Kiswahili |
| 8 | ONU | Kifaransa, Kiswahili |
| 9 | ONU | Kifaransa, Kiswahili |
| 10 | ONGI | Kifaransa, Kiswahili |
| 11 | ONGI | Kifaransa, Kiswahili |


Wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada waliyo shiriki katika huu utafiti walisema shida ingine kuhusu kuripoti muzuri kupitia namba za simu ni kwamba mara mingi watu wenye wanaripoti unyanyasaji wanazungumuza kwa mtu mu troisième personne du singulier ao kutumia maneno ya fumbo (inayo julikana pia kama "maneno iliyo fichwa"). *"Iyi hali inaweza sababisha shida kwa watowa huduma ambao hawana mafunzo kuripoti unyanyasaji wakati kwenye simu* [kwa namba ya simu inayo tumikishwa na jamii yote] *na kuipeleka kwa mtu anaye husika"*, alisema mutumishi wa shirika ya kutowa misaada kutoka Kinshasa. Ni kawaida kwa wahanga inchini Kongo na fasi zingine kuongea kwa zarau wakati wanazungumuza juu ya unyanyasaji wa kingono. [13]Iyi ni hasa wakati wanaume wanaripoti unyanyasaji, kwa sababu ya zarau yenye inasababisha. Mutumishi wa shirika ya kibinadamu alieleza hali moja kama hiyo: *"Nilijua kama ile jambo ilimufikia kulingana na gisi alikuwa anazungumuza na kuitikia, lakini hakuweza kuniambia hapo hapo."*

[13] Tembelea: https://doi.org/10.1371/journal.pone.0174741

*Picha ya 3 : Luga kuu inayo zungumuzwa na wauzuriaji katika utafiti ndani ya jamii*




*Picha ya 4: Luga zingine zinazo zungumuzwa na wauzuriaji katika utafiti ndani ya jamii*



## Siyo kila wakati watu wanajua gisi ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono kwa sababu habari kuhusu namna ya kuripoti haieleweki muzuri

Wahanga, wanamuke na watu ndani ya jamii hawaelewi muzuri vifaa mingi vya kupasha habari kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono. Na iyi hali inatuma watu wengi hawajui gisi ya kuripoti kwa siri vitendo vya zuluma na unyanyasaji wa kingono ili kupata jibu ya muzuri.

### Watu wana changanyikiwa na vifaa vya mawasiliano vinavyo himiza njia mingi tofauti za kuripoti, zingine hazitumiki tena

Mara mingi mashirika zisizo za kiserikali za kimataifa na mashirika ya Umoja wa Mataifa zilianzisha mbinu zao wenyewe za kuripoti kama vile njia za simu na masanduku ya maoni. Kila shirika inatumia mbinu yake ya mawasiliano na vifaa ili kuhimiza kuhusu matumizi. Matokeo yake, markasi mingi za kubandikwa zinaweza kupatikana ndani ya jamii katika mashariki ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (tazama picha ya 5, kwa mfano). Njia za kuripoti zinatumiwa siyo tu juu ya zuluma na unyanyasaji wa kingono lakini pia kwa kutowa maoni na malalamiko ya aina yote.

Wanamuke na wanaume waliyo shiriki katika huu utafiti wanasema wanaona iyi hali inachanganya. Maoni ya mwanaume mumoja mkulima inaonesha kuchanganyikiwa kutokana na ukosefu wa uwazi: "Sijui nipige ku namba gani. Kuko watu mingi sana hapa kijijini." Tatizo ingine ni kwamba namba zimoja za simu zenye zinaandikwa ku makartasi za kubandikwa hazitumiki, na kuko masanduku ya maoni yenye haitumiki tena. Wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada wanazibitisha kwamba mara mingi masanduku ya maoni na makartasi ya kubandikwa hazibanduliwi wakati miradi zinaisha. Hakuna document ya sasa inayo patikana katika jamii – ao kuhusu hiyo jambo kwenye ngazi ya uongozi pa Goma[14] – yenye inaweka wazi namba zote za simu na njia za kuripoti zenye zinapatikana.

Kwa hivyo jamii na watoa huduma hawaelewi muzuri ni namba za simu ngapi za mashirika za kutowa misaada zinatumika katika jamii ndani ya jimbo ya Kivu ya Kaskazini; ni namba gani za simu ni za kuita kwa bure; na ni luga gani zenye watowa huduma kwenye njia za simu wanazungumuza. Katika huu utafiti, tuliita mashirika 23 wanamemba wa PSEA network pa Goma (kwa msaada wa vikundi 43 vya kuakilisha), ambao walitupatia namba 11 za simu.

[14] Kwa sasa hakuna habari kwa kifupi kuhusu njia za kuripoti zenye zinapatikana kwa sasa katika wilaya ya Nyiragongo. Karte ilitayarishwa katika wilaya ya Beni na mtandao ya UNICEF inayo husika na ukingo zidi ya zuluma na unyanyasaji wa kingono (PSEA network).

*Picha ya 5: Markasi za kubandikwa zinatowa maelezo kuhusu namba za simu zilizo wekwa na mashirika ya kibinadamu*




## Watu hawaelewi luga zenye zinatumiwa katika vifaa vya kutowa habari

Mara mingi wanamuke na wanaume katika jamii zinazo lengwa wana pata shida ya kuelewa vifaa vya kutangazia jamii kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono na njia za kuripoti. Markasi mingi za kubandikwa zenye timu iliyo fanya utafiti iliona ndani na kandokando ya jamii kwenye utafiti ulifinyaka ndani ya wilaya ya Nyiragongo zinaandikwa mu Kifaransa. Watu mingi katika iyi eneo hawawezi kusoma Kifaransa na wanaweza kupendelea kusoma Kiswahili ya Kongo (tazama picha ya 3 na 4). [15]Washiriki wengi, hasa wale wasiyo na elimu ya kawaida, wanapendelea kupokea habari mu luga za nyumbani kama Kikumu ao Kinyarwanda.

Mara mingi pia markasi za kubandikwa zina maneno mingi sana (tazama picha ya 5), na kufanya watu wenye hawana elimu kutoelewa. Kuko uwezekano ya kwamba wanamuke mu maeneo ya vijijini walimaliza shule ya msingi ukilinganisha na wanaume ao wanamuke ndani ya miji. Vifaa vya kutowa habari kwa wanamuke katika maeneo ya vijijini vinapashwa kuzingatia njia za mawasiliano zenye abo banapendelea.

[15] Hakuna picha kubwa inayo onesha ginsi kuna manjiya zaku toa tarifa inayo kuwa tayari ndani ya mjini wa Nyiragongo wakati hii imeandika. Muungano wa maasiliano UNICAF/PSEA wamefanya orodha ya utambulisho njini Beni.

## Kutowa habari kwa njia ya michoro inaweza kusaidia lakini mara mingi inatafsiriwa mubaya

Tulionesha washiriki wanaume na wanamuke ndani ya jamii michoro kutoka ku kartasi iliyo tayarishwa na wanamemba wa PSEA network juu ya kuhimiza kuhusu kuripoti kupitia namba ya simu ya ushirikiano wa mashirika (Interagence). Wakati tulipima usikilivu wao, tuligundua kwamba kuko picha kwenye markasi za kubandikwa kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono na vifaa vingine havieleweki muzuri na kutafsiriwa mubaya.

Picha ya 6 ni mfano wa picha yenye ilitafsiriwa mubaya na watu ndani ya jamii. Wanamuke na wanaume wengi ambao tuliomba kutazama hiyo picha waliielewa kama kumaanisha mzozo kuhusiana na haki ya kupokea chakula, siyo kama hali ya zuluma na unyanyasaji wa kingono. Mwanamuke mumoja mufanyabiashara anaye ishi mu kambi ya wakimbizi wa ndani alitafsiri hiyo picha kama yenye inaonesha: *"Huyo binti haiko ku liste ya wenye watapokea. Wazazi wake walimuleta kwa mutumishi wa shirika ya kutowa misaada juu wamuandike".*

*Picha ya 6: Watu ndani ya jamii hawakuelewa picha inayo onesha zuluma na unyanyasaji wa kingono*



Picha zimoya zinaweza pia kuongeza hali ya kulaumiwa kwa wanamuke ambao wanafanya ngono juu ya kupata gisi ya kuishi. Picha ya 7 ilioneshwa kwa kundi ya wanaume wafanyabiashara katika moja ya maeneo kwenye utafiti ulifanyika. Wanaume walisoma hiyo picha kama kuonesha ukahaba ("Ana mutongoza; uyu ni kahaba"), ambayo wanaiona kama "zambi kwa mwanamuke". Kutumia picha kama hizi inaweza kuongeza hali ya kujisikia kuzarauliwa kwa wahanga. Wanamuke mwa hiyo hiyo jamii waliripoti kwamba walisha laumiwa "wakati mutumishi wa shirika ya kibinadamu anawataka kingono na hawawezi kusema hapana". Hali ya kujisikia kuzarauliwa na haya inasababisha sana wanamuke mingi kuamua kutoripoti mahusiano na wafanyakazi wa kibinadamu.

*Picha ya 7: Picha kama hizi zinaweza kuongeza hali ya kujisikia kuzarauliwa kwa wanamuke ambao wanafanya ngono juu wapate gisi ya kuishi*



Picha kuhusu hali ya kulazimishwa na kutokubaliana zinaonekana kueleweka muzuri na wanaume na wanamuke kwa sababu zinazoonesha unyanyasaji wa kingono na kutumiwa kingono. Kwa mfano, picha ya 8 ilieleweka kama kuonesha unyanyasaji wa kingono juu ya gisi sura ya binti inaonekana na kwa gisi nguvu inaonekana kutumiwa. "Huyu kijana anakamata huyu binti kwa kinguvu. Iyi ni unyanyasaji", alisema mwanamuke mumoja mkulima. Ni vigumu kwa picha kama hizi kuwezesha watu ndani ya jamii kuelewa habari kuhusu unyanyasaji wa kingono kama zenye kufanyika bila makubaliano na mara mingi kwa kutumiwa nguvu. Vitambulisho vya wafanyakazi wa mashirika ya kutowa misaada kama magari za jipe (jeeps) za mweupe na ma jilé (gilets) zinaeleweka na watu mingi.

*Picha ya 8: Picha zinaonesha zuluma na unyanyasaji wa kingono kama tendo ya bila makubaliano zilieleweka muzuri*



## Watu wanahitaji kupata habari zinazo faa kuhusu namna ya kuripoti, gisi zinatumika na msaada gani inatolewa

Wanamuke katika maeneo kwenye utafiti ulifanyika wanasema wanahitaji kupata habari zaidi na zinazo faa kwa kuweza kutumia ili waweze kufanya maamuzi muzuri juu ya maisha yao na maisha ya watoto wenye walizala kupitia mahusiano na watumishi wa mashirika ya kibinadamu. Kuliko mashirika ya kutowa misaada ziambiye wanamuke ni tabia gani inakatazwa, wanamuke wanataka kujua ni msaada gani wanaweza kupata kama wanaripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono. Kwa kuongeza, kusema kwamba wahanga wanaweza kuwa wanafanya kitu mubaya inaweza kuleta matokeo mubaya, kwa sababu wahanga wanaweza kuogopa kupata shida kama wanaripoti unyanyasaji.

Mara mingi markasi za kubandikwa siku hizi zinalenga kufasiria kwamba ni mubaya na inakatazwa kuwa na mahusiano wa kingono na watumishi wa mashirika ya kibinadamu, lakini mara mingi hazielezi wazi gisi ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono na ni msaada gani wahanga wanaweza pata. Kartasi ku picha ya 9 ni mfano ya iyi hali. Maandiko ku kartasi ya kubandikwa inasomeka kama: "Kila mtu iko na haki ya kupata msaada ya kibinadamu na haiwezi kubadilishwa kwa kutumia ngono ao faida zingine." Haina ako namba ya simu kwa ajili ya kuripoti. Na iyi ilisababisha washiriki wa utafiti kutoweza kujuwa wapi kuripoti tabia yenye inaelezwa.

*Picha ya 9: Kartasi ya kubandikwa inajulisha jamii juu ya haki yake ya kupata misaada ya kibinadamu bila kuzulumiwa na kunyanyaswa kingono, lakini haitowi maelezo kuhusu fasi ya kuripotia zuluma na unyanyasaji wa kingono*



Wahanga na wengine wanamuke wengine waliyo shiriki katika huu utafiti walisema wanataka kujua ni njia gani za kuripoti zenye wanaweza kutumia; ni nini wanaweza kutarajia kutoka kwa njia hizi na wakati gani; na ni aina gani ya tabia ao jibu wanaweza na wanapashwa kutarajia kutoka kwa wafanyikazi wa mashirika za kibinadamu. Hii ni tofauti sana na kutowa shauri wa gisi mwanamuke anaishi mu hali ya shida ya zarura anapashwa na hapashwi kuwa na hiyo tabia. Wanamuke na wanaume wanatamani kupata hizo habari mu luga za nyumbani na katika mipangilio za kupatikana kwa urahisi.

## Wanaume, vijana na vikundi vingine vyenye kuwa katika hatari havilengwi katika kampeni za uhimizaji kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono na wanaweza wasijue wapi pa kuripoti unyanyasaji

Vifaa vya mawasiliano vinalenga hali ya wanamuke wakubwa waliyo nyanyaswa na kuzulumiwa kingono na wanaume. Wakati habari zenye ziko zinaonesha wanamuke wakubwa ni wahanga wa mara kwa mara wa zuluma na unyanyasaji wa kingono mashariki ya Kongo, siyo tu wenyewe njo wahanga. Wanaume, vijana na wahanga wengine hawalengwi katika juhudi za uhimizaji na vifaa vya kutowa habari. Kushindwa kuhusisha hawa watu wenye kuwa katika hatari inaweza kuongeza unyanyasaji na kujisikia kuzarauliwa na kusababisha vinyume vya muda mrefu kwa afya yao ya kingono, uzazi na akili.[16]

Markatasi za kubandikwa, kwa mfano, haziweki picha za wanaume ao vijana wanaume kama wahanga wa zuluma na unyanyasaji wa kingono, ao kuzungumuzia unyanyasaji unao fanyika na wanamuke, hata hivyo unyanyasaji wa kingono kwa wanaume na vijana wanaume unafanyika sana inchini Kongo, kama katika maeneo zingine zenye mizozo na wakimbizi. Kujisikia na kuweka haya mu roho, boga ya kuzarauliwa, na huduma ambazo hazitambuwi wanaume kama wahanga zinazuwia wanaume mingi wahanga kushindwa kuripoti.[17]

Vivyo hivyo, vijana wanaume na mabinti wako katika hatari kubwa ya zuluma na unyanyasaji wa kingono lakini hawalengwi na mashirika ya kutowa misaada kama watu wenye mahitaji za kipekee kwa kupata habari na njia za mawasiliano. Hata hivyo unyanyasaji wakati wa ujana (adolescence) inaweza kuwa na vinyume katika maisha yote, ikiwemo uwezo kidogo ya elimu na umaskini.[18]

Kuhusisha hawa watu wengine wenye kuwa katika hatari katika uhimizaji na kujaribu kuboresha mawasiliano ni muhimu juu ya kukomesha unyanyasaji. Kwa kuwasaidia wanaume, vijana wanaume na wahanga wengine, mashirika za kutowa misaada zinapashwa jitahidi kupiganisha hali ya kujisikia kuzarauliwa na kutowa habari juu ya gisi wanaweza kuripoti kwa usalama. Hii itahitaji mbinu inayo faa na yenye kulinda usiri, hasa kwa mahusiano kati ya watu wa jinsia moja, ambayo inazoweya kufichwa sana kwa sababu ya ubaguzi na kuogopa kushambuliwa.


### Kushirikiana na wanaume kama watu wenye kusaidia inaweza kuwezesha wanamuke wahanga kuripoti unyanyasaji waliyo fanyiwa na wafanyakazi wa mashirika mingi za kibinadamu

Kujaribu kuboresha mawasiliano haizingatii kuwashirikisha wanaume katika mbinu za kubadilisha tabia zinazo lenga kuzuwia zuluma na unyanyasaji wa kingono na kuwezesha wanaume kuripoti kwa wingi. Wanaume wana jukumu muhimu katika kuwezesha wanamuke mingi kuripoti. Wanamuke na wanaume walituambia kwamba wakati mwanaume anaunga mkono, kuko uwezekano mukubwa wa mwanamuke kuripoti zuluma na unyanyasaji

[16] Tembelea: https://doi.org/10.1371/journal.pone.0174741; https://www.jstor.org/stable/41494485
[17] Tembelea: https://reliefweb.int/sites/reliefweb.int/files/resources/Into_The_Mainstream-Addressing_Sexual_Violence_against_Men_and_Boys_in_Conflict.pdf
[18] Tembelea: https://doi.org/10.1371/journal.pone.0174741

wa kingono. "Inatokana na kama mwanaume iko na mahusiano muzuri na bibi yake", mwanaume mumoja anaye ishi kandokando ya muji alituambia: "Ikiwa ni mahusiano ya muzuri, atasaidia mwanamuke". Baba, wajomba na kaka pia wanaweza kusaidia kwa njia iyi, walisema wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada. Mbinu za kushirikisha zinaweza himiza tabia kama hiyo.

*Picha ya 10: Mara mingi namna wahanga wana ripoti ni tofauti sana na namna yenye wanatarajia*




*Wauzuriaji katika mazungumuzo ya vikundi wali zungumuza kuhusu njia inayo pendelewa na njia inayo wezekana zaidi ya mfano ya muhanga Carine.

## Ili kuboresha hali yenye iko, wanamuke wanataka mashirika ya kutowa misaada kutumika na mashirika ya nyumbani na mipango ya jamii yenye wanajuwa na kuamini

Wanamuke na wahanga wanasema kwamba wanapendelea mashirika ya kutowa misaada kutumika na wanamuke wa Kikongomani na mashirika yenye wanaaminia. Wakati mashirika ya kutowa misaada zinashirikiana na mashirika ya nyumbani kusaidia watu kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono, tunasikia watu mingi wanashuhudia kupata msaada. Moja ya ushuhuda yenye inakumbukwa zaidi ilikuwa ya kiongozi wa jamii wa kike ambaye alisindikiza wahanga wa ubakaji mpaka kwenye kituo cha afya, kutowa msaada kuhusu tabia ya kukamata wakati binti ule aliogopa kutafuta huduma ya afya. "Aliniaminia kwa sababu nililinda siri yake", alisema kiongozi huyo baadaye. (Soma ushuhuda hiyo katika Picha ya 10).

*Picha ya 11: Gisi mfano muzuri inavyo onekana kwa muhanga (mfano ya utafiti)*

***Carine* anaishi katika kambi ya wakimbizi wa ndani (PDI) karibu na mbuga la wanyama ya taifa ya Virunga. Yeye ni mwanafunzi katika shule ya sekondari na alianza mahusiano na mutumishi wa shirika ya kutowa misaada. Alisema angeweza kumusaidia kupata bunga na mafuta zaidi wakati wa mapokezi kama anaitika kufanya ngono naye. Carine aliitika. Lakini ilifikia wakati huyo mutumishi alimunyanyasa na kumubaka na kumupiga. Carine aliogopa kusikia kile kyenye wazazi wake wangesema na kwa hiyo alimwambia kiongozi wa jamii wa mwanamuke mwenye anaaminika jambo yenye ilitokea.***

***"Carine alikuwa mwanafunzi na nilijua ya kwamba wazazi wake wangemuachisha masomo [wangejua kuhusu unyanyasaji]. Alitaka kuifanya siri juu aendelee na masomo", alieleza kiongozi huyo wa wanamuke.* *Aliambia Carine waende naye kwenye kituo cha afya cha karibu ya kwenye Carine anaishi, na wakati wanatembea pamoja alikuwa anahakikisha kubakia mbali kidogo na Carine juu watu wasiwaziye kama wako pamoya. Kwenye kituo cha afya alikuwa anamusemea Carine na kuhakikisha kama anapata dawa. Wakati wazazi wake waligundua, kiongozi huyo alijifanya sawa vile njo ilikuwa mara ya kwanza ana kutanana na Carine.***

**** Carine ni jina ya kutunga. Iyi ushuhuda inatoka kwenye ripoti yenye tulipokea wakati wa utafiti. Tulibadilisha mambo fulani muhimu juu ya kuhakikisha kulinda siri kama gisi tuliahidi.***
***** Kiongozi wa jamii alishiriki katika huu utafiti. Ushuhuda yake ni ya kweli.***

Kwa kujibia iyi ombi kutoka kwa jamii, mashirika zimoja za kimataifa za kutowa misaada ziliunda mbinu ya kushirikiana na mashirika na miradi katika jamii. Iyi ushirikiano inapashwa kuendelea, na inaweka wazi ya kwamba jukumu ya shirika ya nyumbani ni kusaidia muhanga kuliko kupokea ripoti kwa niaba ya shirika ya kimataifa ambayo inatakiwa kushurulikia iyo jambo. Kupitia mipango, wanamuke walisha pata mafunzo juu ya gisi ya kupambana na ubakaji na unyanyasaji wa kingono inayo fanyika na mashirika zinazo tumika kwa kumesha unyanyasaji wa kijinsia. Wanaweza pia kufundishwa kuhusu kuripoti na kuzuwia zuluma na unyanyasaji wa kingono. Mara mingi watowa huduma kama hiyo wanaaminia wanamuke katika jamii na walisha tafutwa wakati wanamuke wanapata shida za kuhusiana na zuluma na unyanyasaji wa kingono. Wakati wanamuke walihusika katika kuchagua watu waliohusika, walisema waliwaaminia.

Kwa kuongeza tabia ya kuripoti, wanamuke walitoa wito kwa mashirika ya kutowa misaada kutowa mafunzo na kusaidia vikundi vya wanamuke vya jamii na kuwapa vifaa kwa kusaidia wahanga wakati wanaripoti. Iyi ni pamoja na kutowa msaada kwa simu za pamoja, mkopo, pesa ya usafiri na malipo kwa watu wenye kujitolea. "Tunajua jamii na tunaweza kukuambia namna muzuri ya kusaidia wanamuke", alisema mwanamuke mumoja mkulima ambaye anashiriki katika muradi wa wanamuke ndani ya moja ya jamii kwenye utafiti ulifanyika. Watu ndani ya jamii na mashirika za nyumbani walipendekeza kwamba mashirika ya kutowa misaada zinapashwa kushirikiana na vikundi vya kijamii na kukamata maamuzi ya pamoja kuhusu gisi musaada unapashwa tolewa. Pia waliona ya kwamba musaada wa kipesa wa muda mrefu utakuwa na maana kwa kuanzisha hizi tabia.

## Wanamuke wanataka kushirikishwa katika kutafuta watu ambao wanaaminika juu ya kuhakikisha siri inalindwa na usalama wakati wa kuripoti

Kusaidia kazi ya jamii mu lengo ya kusaidia wahanga kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono kwa kuchaguwa wawakilishi ndani ya jamii inaweza kusaidia kujenga uaminifu na usalama wa wahanga. Kama ilivyo elezwa hapo mbele, wanamuke wote wenye tulizungumuza nao walipendelea kuripoti uso kwa uso kwa wanamuke wenye wanaaminia. Walituambia hasa ya kwamba wawakilishi kama hao wanapashwa kuchaguliwa na wanamuke na vikundi vingine vyenye kuwa katika hatarini, na kuendelea kushirikiana nao. *"Hapa tunajua nani njo mwakilishi muzuri kwetu na nani siyo muzuri"*, mwanamuke mumoja mkulima alisema.

Iyi ni muhimu, juu kwa sasa siyo njia zote za kuripoti uso kwa uso ziko salama. Wanamuke walisema kwamba kuko watu wenye wanaweka wanamuke katika hatari ya kunyanyasika zaidi. Katika jamii moja wanamuke walihimizwa kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono katika kituo cha afya ambacho kiliwekwa kama sehemu salama. Hata hivyo, watowa huduma za afya katika kituo hicho wangeomba ngono kwa kutowa huduma za afya. Katika eneo ingine ambapo utafiti ulifanyika, wanamuke na wanaume walidai kwamba kiongozi aliomba kufanya ngono na wanamuke wakimbizi wa ndani ili kuwapatia chakula kutoka kwa mashirika ya kutowa misaada. Huyo huyo kiongozi alikuwa kwenye kamati inayo husika kupokea malalamiko iliyo undwa na shirika la kimataifa kwa kushurulikia shida na mahitaji ya watu kupitia masanduku ya maoni.

Kama wahanga wanaripoti kwa shirika ya kijamii, kuendelea kuwa hatari ya shirika hiyo kuonekana tofauti na mashirika ya kimataifa kutokana ao kutokuaminika ndani ya mashirika za kijamii kutokana na majibu zisizo faa kuhusiana ripoti zenye zinatolewa na watu. Kuliko hivyo, njia ya kutumikishwa na jamii kwa kusaidia wahanga wenye wanaripoti inaweza uaminifu wenye wanamuke wanataka bila kuficha wapi kwenye kosa inatokea.

## Wanamuke hawahitaji tu habari juu ya gisi ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono lakini pia kujitegemea kipesa ili kuepuka kunyanyasiwa

Watumishi wa mashirika ya kibinadamu waliyo hojiwa walionesha muzuri sana upungufu katika njia inayo tumiwa kwa sasa, lakini utafiti uligundua shida kubwa na maelewano kati yabo na watu ndani ya jamii kuhusu suluhisho ambazo zinapendelewa. Wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada wanatoa wito wa kusaidia kufanyika kwa *"uhimizaji"*, lakini jamii zinasema zinahitaji msaada wa kupunguza umaskini ili kukomesha zuluma na unyanyasaji wa kingono. Walijua kabisa kwamba mahusiano ya unyanyasaji inayo fanyika na wafanyakazi wa mashirika za wanaadamu haitakiwi.

Wafanyakazi mingi wa mashirika za kutowa misaada wanaamini kwamba suluhisho kumesha kiwango cha juu cha zuluma na unyanyasaji wa kingono ni: *"kuongeza uhimizaji kuhusu unyanyasaji wa kingono na njia za kuripoti"*. Mutumishi mumoja wa shirika ya kutowa misaada pa Goma alitowa maoni yake katika mazungumuzo na wengine: *“Wanamuke hapa hawaoni kama ni tatizo kufanya mapenzi na mutumishi wa shirika la kibinadamu. Ni kukosa kujuwa. Tunapashwa kuongeza uhimizaji”.*

Utafiti wetu, hata hivyo, unaonesha ya kwamba ni mubaya kutozingatia mbinu za wanamuke wa Kongo za kutafuta maisha. Haiweki wazi matatizo za msingi ambazo wanamuke wanapata katika kuhudumia familia zao. Haikubali pia kazi ya shirika ya wanamuke na sehemu ya jukumu ambayo mashirika za kutowa misaada katika chaguo zenye wanapewa.

Wanamuke wote wenye tulizungumuza nao katika jamii, ikiwemo wahanga, waliomba kupata msaada wa kipesa kwa ajili ya kuzuwia zuluma na unyanyasaji wa kingono. Walisema wanamuke hawahitaji kuanza mahusiano na wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada kama wana jitegemea kipesa. Wanamuke wanataka mashirika za kutowa misaada kutowa mikopo ya biashara ndogo ndogo ao msaada wa kipesa kama njia ya kuzuwia.

## Shukrani

Tunataka kutowa shukrani zetu za zati kwa wote waliyo shiriki katika utafiti kwa kutupatia muda wao na kwa ujuzi wao. Huu utafiti haungefanyika bila mchango wenu. Aksanti sana!

Huu tafiti uliongozwa na shirika la Watafsiri wasiyo kuwa na Mipaka/CLEAR Global. TWB inataka kuwashukuru watafiti kutoka “Cellule d'Analyse Intégrée” ya UNICEF ambao walisaidia na kushiriki katika kazi za kukusanya habari zenye ubora.

Huu utafiti ulirahisishwa kwa muchango wa wanamemba wa PSEA network pa Goma. Kamati ya Kimataifa ya kusaidia (IRC) ilisaidia kupanga na kurahisisha kazi ya utafiti katika wilaya ya Nyiragongo. Mahojiano na wahanga wa unyanyasaji uliyo fanyika na mashirika za kibinadamu zenye tunashirikiana nazo ziliendeshwa kwa ushirikiano na Sauti Ya Mama Mukongomani. Tunawashukuru wote wenye walishirika kwa kuchangia ujuzi na kutowa musaada wao.

Huu tafiti ulifaziliwa na Shirika la Afya Duniani pa Geneva na kuungwa mkono na PSEA network wa OMS mashariki ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Timu iliyo fanya utafiti inawashukuru wenzake kutoka OMS pa Goma, Kinshasa na Geneva kwa msaada wao.

## Vyanzo vilivyo tumiwa


Autesserre, S. (2012). "Dangerous Tales: Dominant Narratives on the Congo and their Unintended Consequences," African Affairs, 111 (443), pp. 202-222. https://www.jstor.org/stable/41494485

Barter, C., Renold, E., (1999). The Use of Vignettes in Qualitative Research. Social Research Update, Iss. 25. https://sru.soc.surrey.ac.uk/SRU25.html

Blau, L., (2017). Victimizing those they were sent to protect enhancing accountability for children born of sexual abuse and exploitation by UN Peacekeepers. https://jilc.syr.edu/wp-content/uploads/2018/04/Blau_Macro_Complete20170321.pdf

Bolton, L. (2020). Barriers to education for girls in the Democratic Republic of Congo. K4D Helpdesk Report 750. Brighton, UK: Institute of Development Studies. https://resource-centre-uploads.s3.amazonaws.com/uploads/750_barriers_to_education_for_girls_in_drc.pdf

Congo Research Group (2021). Kivu Security Tracker. Human Rights Watch, New York University's Center on International Cooperation. https://kivusecurity.org/

Chynoweth, S., Freccero, J. & Touquet, H. (2017). Sexual violence against men and boys in conflict and forced displacement: implications for the health sector. Reproductive Health Matters, Iss. 25:51, pp. 90-94. https://www.tandfonline.com/doi/full/10.1080/09688080.2017.1401895

Dolan, C. (2014). Into the Mainstream: Addressing Sexual Violence Against Men and Boys in Conflict. Overseas Development Institute, https://reliefweb.int/sites/reliefweb.int/files/resources/Into_The_Mainstream-Addressing_Sexual_Violence_against_Men_and_Boys_in_Conflict.pdf

FIDH (2013). DRC: Victims of Sexual Violence Rarely Obtain Justice and Never Receive Reparation. Major changes needed to fight impunity. FIDH. https://www.fidh.org/IMG/pdf/rapport_rdc_.pdf

Graça Machel Trust (2021). Women's Financial Inclusion in the Democratic Republic of Congo. New Faces, New Voices & IDRC CRDI. https://idl-bnc-idrc.dspacedirect.org/bitstream/handle/10625/59153/59307.pdf

ICRC (2006). Democratic Republic of the Congo. Practice relating to Rule 93. Rape and Other Forms of Sexual Violence. IHL Database. https://ihl-databases.icrc.org/customary-ihl/eng/docs/v2_cou_cd_rule93

Inter-Agency Standing Committee (IASC) (no date). Global implementation of PSEA in humanitarian response (Congo). IASC. https://psea.interagencystandingcommittee.org/dashboard

Inter-Agency Standing Committee (IASC) (2016). Guidelines. Inter-agency community-based complaints mechanisms. Protection against Sexual Exploitation and Abuse. IASC. https://interagencystandingcommittee.org/system/files/2021-03/Best%20Practice%20Guide%20Inter%20Agency%20Community%20Based%20Complaint%20Mechanisms.pdf

ITUC International Trade Union Confederation (2011). Violence against Women in Eastern Democratic Republic of Congo: Whose  Responsibility? Whose Complicity? IPIS Research. https://www.ituc-csi.org/IMG/pdf/ituc_violence_rdc_eng_lr.pdf.pdf

Matti, S. (2015). Governing sexual behavior through humanitarian codes of conduct. Disasters - Overseas Development Institute, Vol. 39, Iss. 4, pp. 626-647. https://onlinelibrary.wiley.com/doi/abs/10.1111/disa.12128

McAlpine, A., Hossain, M. & Zimmerman, C. (2016). Sex trafficking and sexual exploitation in settings affected by armed conflicts in Africa, Asia and the Middle East: systematic review. BMC Int Health Hum Rights Vol, 16, Iss. 34. https://doi.org/10.1186/s12914-016-0107-x

Reliefweb (2021). DR Congo: Volcano Nyiragongo – May 2021. Reliefweb https://reliefweb.int/disaster/vo-2021-000059-cod

Samarasekera, U. (2021). Experts critise WHO response to sex abuse allegations. The Lancet, Vol. 398, Iss. 10308, pp. 1291-1293. https://www.thelancet.com/journals/lancet/article/PIIS0140-6736(21)02214-5/fulltext

Sida (2014). The Rights of LGBTI People in the DR of Congo. Sida. https://cdn.sida.se/app/uploads/2021/05/07083458/rights-of-lgbt-persons-drc.pdf

Social Sciences Analytics Cell (CASS). (2021). Perceptions around Sexual Exploitation and Abuse (SEA) and barriers to community-based reporting. Equateur Province, DRC. UNICEF. https://www.unicef.org/drcongo/media/5901/file/COD-CASS-Equateur-PSEA-EN-correction.pdf

Spangaro J., Adogu, C., Ranmuthugala, G., Powell Davies, G., Steinacker, L., Zwi, A. (2013). What Evidence Exists for Initiatives to Reduce Risk and Incidence of Sexual Violence in Armed Conflict and Other Humanitarian Crises? A Systematic Review. PLoS ONE 8(5): e62600. https://journals.plos.org/plosone/article?id=10.1371/journal.pone.0062600

Stark L., Sommer, M., Davis, K., Asghar, K., Assazenew Baysa, A., Abdela, G., et. al. (2017). Disclosure bias for group versus individual reporting of violence amongst conflict-affected adolescent girls in DRC and Ethiopia. PLoS ONE 12(4): e0174741. https://doi.org/10.1371/journal.pone.0174741

Stark, L, Seff, I., Reis, I., (2020). Gender-based violence against adolescent girls in humanitarian settings: a review of the evidence. The Lancet Child & Adolescent Health. Vol. 5. Iss. 3., pp. 210-222. https://www.sciencedirect.com/science/article/abs/pii/S2352464220302455

United Nations (UN) (2016). Glossary on Sexual Exploitation and Abuse. Thematic Glossary of current terminology related to Sexual Exploitation and Abuse (SEA) in the context of the United Nations. https://reliefweb.int/sites/reliefweb.int/files/resources/un_glossary_on_sea.pdf

## Kiambatisho 1: Vifupisho

| | |
|---|---|
| AVEC | Mashirika za vijijini ya akiba na mkopo |
| EAS | Unyanyasaji wa kingono |
| FGD | Mazungumuzo ya kikundi |
| IDI | Mahojiano ya kindani |
| IRC | Kamati ya Kimataifa ya kusaidia |
| KII | Mahojiano na mushiriki muhimu |
| MONUSCO | Tume ya Umoja wa Mataifa ya uimarishaji inchini Kongo |
| OMS | Shirika la Afya Duniani |
| ONG | Shirika isiyo ya kiserikali |
| ONGI | Shirika ya kimataifa isiyo kuwa ya kiserkali |
| ONU | Umoja wa Mataifa |
| PDI | Mkimbizi wa ndani |
| PEAS | Kukingwa na zuluma na unyanyasaji wa kingono |
| RDC | Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo |
| SEAH | Zuluma na unyanyasaji wa kingono |
| TWB | Shirika la Watafsiri wasiyo kuwa na Mipaka |
| UNICEF | Mfuko wa Umoja wa Mataifa kwa Ajili ya Watoto |

## Kiambatisho 2: Ukusanyaji wa habari katika utafiti

Utafiti ulitumia vifaa mbalimbali vyenye ubora. Kwanza, tulitafuta na kukusanya kwa haraka habari kuhusu mada ya utafiti. Mbili, tulitayarisha kwa haraka karte ya luga, mipangilio na njia za kutowa habari kuhusu kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono na njia zenye zinatumiwa na mashirika ya kutowa misaada mashariki ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Tatu, ukusanyaji wa habari za msingi na watu ndani ya jamii, wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada na wahanga wa unyanyasaji wa kingono ilifanyika katika mazungumuzo ya vikundi na mahojiano fupi iliyo pangwa.

### Vifaa vya utafiti

Timu iliyo fanya utafiti ilitumia vifaa vya utafiti vifwatavyo:

#### Kusoma habari kuhusu mada ya utafiti

Google Scholar ilitumikishwa kwa kupata habari kuhusu mada ya utafiti. Kiongozi wa utafiti alitafuta na kukusanya habari za kisomi zilizo tangazwa na habari za maana kutoka mashirika ya kutowa misaada zinazo tumika hasa inchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Maneno yafwatayo zilitumikishwa: unyanyasaji, msaada, mzozo, Kongo, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kuzulumiwa, unyanyasaji, msaada wa kibinadamu, wafanyakazi wa shirika za kibinadamu, walinda amani, Kukingwa na zuluma na unyanyasaji wa kingono, ubakaji, kuripoti, unyanyasaji na kuzulumiwa kingono, zuluma na unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa kingono, unyanyasaji wa kingono, Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara, ONU. Kutokana na muda kidogo, habari kuhusu mada ya utafiti zilikusanywa kutoka tu katika makala (articles) iliyo tangazwa mu kipindi ya miaka kumi iliyopita mu luga Kingereza.

#### Karte

Timu iliyo fanya utafiti ilitayarisha liste ya namba za simu na njia zingine ambazo mashirika ya kibinadamu zinahimiza kwa kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono mashariki mwa Kongo. Hiyo liste ilitayarishwa kwa msaada wa PSEA network pa Goma, ambao ulitoa liste ya mashirika ya kutowa misaada zinazo jihusisha kuhusu kukingwa na unyanyasaji, kutumiwa, kuzulumiwa kingono mashariki ya Kongo. Namba zingine za simu zilipatikana kwa kukagua vifaa za mawasiliano vilivyo himizwa mashariki ya Kongo, kwa kusaidiwa na kutafuta habari ku internet. Kisha mwanamemba kwenye timu aliita namba za simu na kugundua luga zenye zina tumikishwa.

## Ukusanyaji wa data za msingi

Timu iliyo fanya utafiti ilisafiri kwenda mashariki ya Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo mwisho wa Novemba/ Desemba. Shuruli za utafiti yenye ubora ambazo zilishirikisha watu 124 zilifanyika kwa kipindi cha juma tatu (tazama ubao wa 1). Vifaa vya utafiti vilitayarishwa kwa namna ambayo wahanga hawakuombwa kufichiwa hali ya unyanyasaji yenye walipitia. Maulizo ya mahojiano zilitayarishwa kwa kutumia vielelezo na picha za watu wa kutunga. Vielelezo na picha zinatumiwa katika utafiti yenye ubora ili kutoa njia isiyo ya kibinafsi na isiyo ogopesha sana kwa kuongelea mada yenye utata.[19]

## Maeneo ambapo

Utafiti yenye ubora ulifanyika katika wilaya ya Nyiragongo, jimboni Kivu ya Kaskazini, katika jamii mbili tofauti. Hizi jamii mbili zote ziliguswa na muripuko wa volkano ya Nyiragongo mwezi wa tano 2021 na kupokea misaada ya zarura kutoka kwa mashirika mbalimbali ya kibinadamu. Muripuko wa volkano ulipelekea karibu watu 450 000 kuhama. Jamaa mingi zinaendelea kuishi katika makao ya muda kwa musaada wa mashirika ya kutowa misaada na serkali ya Kongo.

Jamii mbili ambapo utafiti ulifanyika zilichaguliwa kwa kushauriana na OMS, PSEA network, Kamati ya Kimataifa ya kusaidia (IRC) na Cellule d'Analyse Intégrée (CAI) ya UNICEF. Hizi maeneo zilichaguliwa kwa sababu wawakilishi wa hizi mashirika walikuwa wana fahamishwa kuhusu shida kuhusiana na zuluma na unyanyasaji wa kingono katika eneo hiyo. Kuchaguwa eneo ilitokana pia na kanuni za ukingo na usalama za IRC, kwa kuwa IRC ilitowa msaada wa usalama katika huu utafiti. Majina za jamii hazijatajwi katika iyi ripoti, kulingana na maombi kutoka kwa viongozi wa serkali wa hizo maeneo na viongozi wa kitamaduni.

Jamii ya kwanza ambapo utafiti ulifanyika (eneo ya 1) inapatikana ku mupaka wa mbuga la wanyama ya taifa ya Virunga na kwa inateseka kwa muda mrefu na ukosefu wa usalama na vurugu yenye kutumia silaha. Iyi jamii iliguswa sana na muripuko wa volkano ya Nyiragongo mwaka 2021. Lave ya volkano iliharibisha vijiji jirani na sasa maelfu ya wakimbizi wa ndani (PDI) wanaishi katika iyi jamii mu kambi isiyo rasmi. Watu ambao wanaishi ndani ya kambi wanapatikana mu hali ya shida na wakaaji wa iyi jamii wanaishi pia mu hali mubaya bila kuwa na kazi za kawaida. Wakimbizi na jamii wanaishi kutokana na mlimo wa kujibu tu ku mahitaji ya kawaida.

Jamii ya pili ambapo utafiti ilifanyika (eneo ya 2) inapatikana pembeni ya muji mkuu wa jimbo ya Kivu ya Kaskazini, Goma (tazama karte ya 2). Goma ni eneo ya biashara inayo hudumia Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uganda na Rwanda, na wakaaji mingi wa eneo ya 2 wanaishi kutokana na biashara na mlimo wa kujibu tu ku mahitaji ya kawaida.. Mauaji na vurugu yenye kutumia silaha ni shida yenye inazowea kutokea, hasa busiku. Kikosi cha kulinda amani cha MONUSCO kinapatikana karibu na wakimbizi wa ndani wanaishi ndani ya hiyo jamii. Watu waliyo kimbia muripuko wa volkano wanaendelea kuishi ndani ya mahema za hali mubaya bila kupata maji safi ya kunywa.

Wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada ambao walishiriki katika utafiti wanahusika katika shuruli ya kutowa huduma za kibinadamu mu jimbo yote ya Kivu ya Kaskazini, ikiwemo jamii katika wilaya ya Nyiragongo na Beni.

---

[19] Tembelea: https://sru.soc.surrey.ac.uk/SRU25.html

## Echantillon na mbinu ya kuichaguwa

Kutumia mbinu ya kuchaguwa échantillon sampuli kulingana na umri, eneo na ukaribu, timu iliyo fanya utafiti alizungumuza na watu 124 (tazama ubao ya 1). Watu wenye wanaishi katika makao ya wakimbizi wa ndani na wakaaji ndani ya jamii walialikwa kushiriki.[20]

Kwa kuelewa muzuri namna gani njia ambazo zinapatikana kwa ajili ya kuripoti zuluma na unyanyasaji wa kingono watafiti walihoji pia wafanyikazi 18 wa mashirika za kibinadamu ambao wanahusika katika mambo kuhusu zuluma na unyanyasaji wa kingono mashariki ya Kongo. Wanatumika katika aina mbalimbali za mashirika ya kibinadamu, ikiwa ni pamoja na ONGI, ONG, mashirika za kirai na Umoja wa Mataifa. Kila mtu iko na jukumu katika ukingo wa kibinadamu zidi ya zuluma na unyanyasaji wa kingono – ikiwemo kujibu malalamiko, kazi ya kuzuwia na kuwaelekeza na kuwasaidia wahanga. Majukumu nao ni kufanya uchunguzi na kuwakilisha wahanga mbele ya vyombo vya sheria.

Kwa kushirikiana na Sauti Ya Mama Mukongomani, timu iliyo fanya utafiti ilifanya pia mahojiano ya kindani na wahanga kumi wa zuluma na unyanyasaji wa kingono uliyo fanyika na wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada katika wilaya ya Nyiragongo. Sauti Ya Mama Mukongomani ni shirika isiyo ya faida ya Kongo inayo fanya kazi katika kujenga amani na kupambana na unyanyasaji wa kijinsia mashariki ya Kongo. [21]Shirika hii inatowa msaada wa moja kwa moja wa kisheria kwa wahanga wa unyanyasaji wa kibinadamu, unayo fanyika pia na watumishi wa mashirika ya kibinadamu. Watowa huduma wa kike ambao wanawasiliana tayari moja kwa moja na wahanga walipewa mafunzo kuhusu mbinu na vifaa vya utafiti. Kisha walifanya mahojiano ya mbali kwa kusaidiwa na watafiti wa TWB.

*Picha ya 12: Washiriki katika utafiti ndani ya kila eneo kwenye utafiti ulifanyika*

| **Kifaa** | **Aina** | **Wilaya ya Beni** | **Wilaya ya Nyiragongo** | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Beni** | **Goma** | **Eneo ya 1** | | **Eneo ya 2** | | |
| | | | | **PDI** | **Wakaaji** | **PDI** | **Wakaaji** | |
| FGD | Wanamuke (miaka 18 mpaka 25) | | | 5 | 5 | 5 | 4 | 19 |
| | Wanaume (miaka 18 mpaka 25) | | | 4 | 5 | 2 | 6 | 17 |
| | Wanamuke (zaidi ya miaka 25) | | | 12 | 7 | 5 | 6 | 30 |
| | Wanaume (miaka zaidi ya 25) | | | 1 | 9 | 5 | 5 | 20 |
| KII | Watowa huduma | | | 1 | | | 1 | 2 |
| | Viongozi wa jamii | | | | 4 | | 2 | 6 |
| | Wafanyakazi wa mashirika za kutowa misaada | 2 | 16 | | | | | 18 |
| IDI | Wahanga | | 10 | | 2 | | | 12 |
| **Jumla** | | **2** | **26** | **23** | **32** | **17** | **24** | **124** |

[20] IRC iliandaa shuruli za utafiti katika maeneo mbili ya utafiti na kuchagua washiriki kulingana na kanuni zilizo tolewa na timu ya utafiti.
[21] https://smmukongomani.org/

## Kuzingatia kanuni muhimu

Utafiti juu ya mada yenye utata kama unyanyasaji wa kingono inahitaji ulinzi wa kipekee ya washiriki. Tulichukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kanuni muhimu za utafiti zinafwata kwa kushirikiana na washiriki katika utafiti wenye kupatikana katika mazingira ngumu:

- Kwa ngambo moja, watafiti waliyo fanya utafiti walichaguliwa kutokana na uzoefu wao katika kufanya utafiti juu ya mambo isiyo ongelewa kwa urahisi kuhusiana na jinsia na unyanyasaji na walifundishwa juu ya kanuni muhimu kwa kuweza kuzungumuza na washiriki katika utafiti wenye kupatikana katika mazingira ngumu.

- Vifaa vya utafiti vilitayarishwa kwa namna ambayo wahanga hawakuombwa kufichua hali ya unyanyasaji yenye walipitia. Kama muhanga hakutaka kuripoti habari, mutumishi kutoka IRC ao Sauti Ya Mama Mukongomani mwenye alipatikana pale kutowa huduma kabla ya huduma ya kwanza.

- Mbinu ya utafiti iliwasilishwa na kurekebishwa na PSEA network inchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hii ilimaanisha kuwa watafiti wanaweza kuwaelekeza wahanga kwa mashirika ya kutowa misaada – walipo ombwa kufanya hivyo na washiriki, kwa kuhakikisha usiri kila wakati wa kuripoti.

- Watowa huduma kutoka IRC na Sauti Ya Mama Mukongomani walihoji wahanga wenye walikuwa wanaaminia, kwa kusaidiwa kwa mbali na timu ya TWB. Iyi hali ilipelekea kutofichuwa majina ya wahanga kulingana na gisi mashirika ya kutowa zilikuwa zinawaahidia kuhusu kulinda siri zao.

## Mapungufu

Kufanya mahojiano na wahanga kupitia mashirika zinazo towa huduma moja kwa moja kwa wahanga wa unyanyasaji wa kingono inaweza kuwa ilisababisha mapungufu katika shuruli ya kuripoti kwa sababu hizo mashirika zinategemea msaada kutoka kwa wafazili. Inaweza pia kusababisha watu waliyo hojiwa kutopana zingine habari zenye wangependelea kuripoti. Ili kupunguza iyi hatari, mbinu mbalimbali zilichukuliwa, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kindani kwa timu ya kufanya utafiti kwa ajili ya kupata ujuzi wa kuendesha mahojiano kuhusu mada yenye utata. Kufanya mazungumuzo ya kindani kisha kukusanya habari na kutumia miongozo ya mahojiano iliyo pangwa ilipelekea kuendelea kupata maoni ya waliyo hojiwa na kutowa kuwasaidia. Kwa kutumia hizi mbinu zenye ziko timu iliyo fanya utafiti iligunduwa ya kwamba iyi hatari ilipunguka.